# UANAZUONI WA MWALIMU NYERERE


512

KAVAZI LA MWALIMU NYERERE
NYERERE RESOURCE CENTRE

# UANAZUONI WA MWALIMU NYERERE

**Wahariri: Saida Yahya-Othman na Bashiru Ally**

**Kavazi Occasional Papers, No. 2**
**2015**

Kimechapishwa na Kavazi la Mwalimu Nyerere

Toleo la kwanza 2015
Chapisho la Pili 2018

© Kavazi la Mwalimu Nyerere

Uanazuoni wa Mwalimu Nyerere/Wahariri: Saida Yahaya-Othman na Bashiru Ally

Kitabu hiki kimechapishwa kwa hisani ya Rosa Luxembourg Foundation (RLS inafadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Ujerumani)

Kimechapwa na Inter Press of Tanzania Ltd., Dar es Salaam

ISBN:  978-9976-9903-0-0

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| Dibaji | Hassan Mshinda | v |
| Misingi ya Falsafa ya Mwalimu | Issa Shivji | 1 |
| Mwalimu: Mwanazuoni Mkanushi | Saida Yahya-Othman | 11 |
| Mwalimu Mshairi | M. M. Mulokozi | 19 |
| Nyerere, Mmajumui wa Kiafrika | Ng’wanza Kamata | 27 |
| Marejeo | | 40 |

*Kazi nia yake si kuleta maendeleo katika aibu, bali ni kuleta maendeleo kwa heshima. Hicho [utumwa] ni kitu cha kwanza kilichovunja heshima ya kazi. Kitu cha pili kilichovunja heshima ya kazi ni ubepari. Utumwa – mtu anammiliki mtu. Ubepari - japokuwa unadhaniwa ni mzuri zaidi kwani unadhaniwa kwamba si utumwa lakini ni vigumu zaidi kuueleza. Katika kazi ya heshima, kazi tunayofanya, tunatumia vyombo kama vile jembe, shoka na panga. Baadae mambo yanaendelea tena tunaweza tukatumia mashine; binadamu anatengeneza hivi vyombo na baada ya kuvitengeneza anavitumia katika kazi yake. Hiyo ndiyo kazi ya kawaida ambayo inajulikana. Mnaoamini Mungu ndiyo kazi aliyotaka Mungu au mnaoamini maumbile hivi hivi basi ndiyo iliyotakiwa na maumbile. Binadamu anatumia vyombo, kama hana vyombo kwake anaazima kwa mwenzie; bwana wewe una mashoka mawili tafadhali niazime kwani leo sina shoka. Ananiazima shoka nikafanyie kazi kwani inajulikana shoka ni kitu anachotumia binadamu kufanyia kazi. Mabepari wamegeuza hii, kwani mashoka yanaazima watu – (kicheko) kwani badala ya watu kuazima mashoka, yao yanaazima watu kwani yamekaa pale pale.*

*Yeye anasema, "Wewe una watu yahe, niazime". Basi mashoka yanaazima watu, kwani kuna kitu kinaitwa capital kinatafuta labour.*

- Mwalimu Nyerere 1967
(akiongea na TANU Study Group)

# DIBAJI

Karibu asilimia 85 ya Watanzania wa leo hawakupata nafasi ya kumuona Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mbali na hotuba zake chache zinazosikika mara kwa mara kwenye vyombo vya habari, ni wachache sana ambao wamepata nafasi ya kusoma maandishi yake kwa undani. Hivyo basi, wengi wa vijana wetu leo hii, hawajapata nafasi ya kumuelewa vizuri Mwalimu Nyerere na falsafa yake ya uongozi na mambo ya msingi aliyoyasimamia kama Baba wa Taifa letu.

Wanazuoni wa Kitanzania wakiongozwa na Prof. Issa Shivji wanawasilisha sehemu ya matokeo ya mradi wa utafiti juu ya fikra za kisiasa za Baba wa Taifa unaogharimiwa na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia. Lengo kuu la mradi huu ni kuandika kitabu juu ya maisha ya Baba wa Taifa. Baada ya uandishi kukamilika, kitabu hicho kitakuwa ni cha kwanza cha kina kuandikwa na Watanzania. Hadi leo vitabu vyote vilivyoandikwa juu ya maisha ya Mwalimu ni vya wageni.

Katika kitabu hiki, waandishi wanamuelezea Baba wa Taifa kama mwanafalsafa, mwanazuoni, mshairi na pia mmajumui wa Kiafrika. Ninashukuru na kufurahi kupata fursa ya kuandika utangulizi wa kitabu hiki kama sehemu ya mwanzo ya kuwasilisha matokeo ya utafiti juu ya maisha ya Baba wa Taifa kwa Watanzania na wasomaji wengine wa Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanatoa nafasi kwa makundi mbalimbali ya jamii yetu kumuelewa Mwalimu kwa njia rahisi na nzuri zaidi; miongoni mwa makundi hayo ni wanasiasa na viongozi wanaochipukia hivi sasa na vijana wenye kutaka maendeleo ya kweli ya Taifa letu. Ni fursa nzuri pia kwa watafiti na wanazuoni kuelewa misingi ya misimamo ya Mwalimu ambayo inaweza kuwa ni nyenzo nzuri ya kufanya utafiti, machocheo, uchambuzi na udadisi anuai. Kwa Watanzania wachache ambao

walikuwepo wakati wa uongozi wa Mwalimu hii ni nafasi nzuri kwao ya kujikumbusha na kutafakari baadhi ya mambo yaliyotokea wakati huo na misingi ya misimamo yake.

Kama nilivyoeleza mwanzo, huu ni miongoni mwa miradi mingi ya utafiti inayogharimiwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia. Tuna furaha kueleza kwamba mradi huu umesababisha kuanzishwa kwa Kavazi la Mwalimu litakalokuwa na sehemu maalum ya kuhifadhi nyaraka na machapisho mbalimbali zilizokusanywa wakati wa utafiti. Kavazi pia litakuwa jukwaa la kuendesha majadiliano na mafunzo kwa watafiti na watu wengine mbalimbali. Tumeona ni bora kuwa na Kavazi ambalo halitahifadhi machapisho juu ya Mwalimu kama maktaba tu, bali litakuwa na shughuli nyingine ambazo kwa njia moja au nyingine zinaweza kuhuisha misingi ya falsafa na misimamo yake.

***Dkt. Hassan Mshinda***
Mkurugenzi Mkuu
Tume ya Sayansi na Teknolojia

12 Novemba 2015

# Misingi ya Falsafa ya Mwalimu

***Issa Shivji***
*Mkurugenzi*
*Kavazi la Mwalimu Nyerere*
*Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)*
*issashivji@gmail.com*

Ingawa Mwalimu alikuwa mwanasiasa aliyeongoza mapambano ya ukombozi wa nchi yake Tanganyika, na baadae Tanzania, yeye mwenyewe aliongozwa na falsafa maalum. Falsafa yake ndiyo iliyozaa itikadi ya kijamaa ya chama chake na maadili yake binafsi. Kwa hivyo, maadili ya Mwalimu yalijikita kwenye falsafa yake na itikadi ya chama chake na sio vinginevyo. Ni muhimu kusisitiza jambo hili hasa katika nyakati hizi ambapo wengi wanahubiri maadili kama kwamba maadili yanaweza kuelea juujuu bila kuwa na mizizi katika falsafa na itikadi.

Msingi mkuu wa falsafa ya Mwalimu ni 'usawa wa binadamu'. Dhana ya usawa sio ngeni hata kidogo katika mitazamo ya falsafa na siasa mbalimbali. Utafutaji wa usawa wa binadamu ndio umeongoza mapambano ya watu na jamii mbalimbali kwa karne karibu kumi. Katika karne hii ya 21, ukiachilia mbali mafashisti, wabaguzi wa rangi na dini, na wale wenye mrengo wa kulia, hakuna mtu ambaye anaweza kukiri, kwa uwazi, kwamba haamini katika usawa wa binadamu. Hata hivyo, mapambano ya usawa bado yanaendelea kwa sababu tafsiri ya dhana ya usawa hutofautiana katika mitazamo ya kifalsafa. Na katika hali halisi ya jamii zetu kote duniani bado kuna mapungufu mengi ya mfumo ambao huendeleza hali ya kutokuwa na usawa. Ndio maana ni muhimu kuelewa kwa undani dhana ya usawa ya Mwalimu.

Fikra za usawa za Mwalimu zilianza mapema katika maisha yake. Akiwa Makerere mnamo mwaka 1944 aliandika barua kwenye

gazeti la *The Standard* chini ya jina la kubuni la JUKANYE akipinga utawala wa kikoloni ambao ulijikita kwenye msingi wa kutokuwa na usawa; yaani Wazungu waliotawala hawakuwa sawa na Waafrika waliotawaliwa. Vilevile aliandika insha yake ndefu ya kwanza juu ya usawa wa kijinsia. Inaelekea msukumo mkubwa katika kuandika insha hii ilikuwa hisia zake mwenyewe alizozijengea kutokana na hali halisi ya mama yake mzazi. Mwalimu mwenyewe aliwahi kukiri kwamba alikuwa karibu sana na mama yake kuliko baba yake. Akiwa mtoto mdogo alifuatana na mama yake akienda shambani kulima na yeye mwenyewe akichunga mifugo. Hata hivyo, fikra zake juu ya dhana ya usawa zilikuwa bado hazijaiva vizuri.

Bila shaka fikra zake juu ya dhana ya usawa zilianza kupevuka alipokutana na maandishi mbalimbali ya wanafalsafa wa kizungu akiwa masomoni katika Chuo Kikuu cha Edinburgh. Aliwasoma akina Hobbes na Rousseau; alitafakari juu ya falsafa ya akina Adam Smith na John Stuart Mill na hatimaye pia alifundishwa nadharia za utawala katika nchi za Magharibi hususan mfumo wa demokrasi ya uwakilishi. Mwandishi wa wasifu wa Mwalimu, Thomas Molony, anadai kwamba mtazamo mzima wa kifalsafa wa Nyerere ulijikita kwenye falsafa ya Magharibi.[1] Hii sio sahihi kwa asilimia mia moja. Bila shaka falsafa hizi za mtazamo wa Kimagharibi zilimuathiri, lakini pia kulikuwa na hali halisi ya jamii yake ambayo pia ilikuwa na mchango wake. Ndio maana, kama nitakavyoeleza baadae, dhana yake ya usawa wa binadamu inaenda mbali zaidi ukilinganisha na dhana ya usawa katika falsafa ya kibwanyenye.

Utafiti wetu unaonyesha kwamba mara ya kwanza ambapo Mwalimu alijidadisi na kujenga hoja zake juu ya dhana ya usawa ilikuwa katika makala yake yaitwayo "Watu Wote ni Sawa?" Ingawa hatuna hakika, inaelekea makala haya yaliandikwa mwishoni mwa

[1] Marejeo yote yako mwisho wa kitabu.

miaka ya hamsini. Kwa kadri tujuavyo, makala haya hayajawahi kuchapishwa na labda Mwalimu hakuwa na nia ya kuyachapisha. Hii ni kwa sababu, jinsi yalivyoandikwa, inaelekea madhumuni yake yalikuwa kufafanua na kujenga hoja kwake yeye mwenyewe juu ya fikra zake juu ya usawa. Kulingana na uchambuzi wetu, makala haya yana umuhimu wa kipekee katika ukuaji wa fikra za kifalsafa za Mwalimu.

Makala yenyewe yamegawanyika katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza, akitumia mtindo wa kujidadisi, (yaani mtindo wa Kisokrati (Socratic method) ambao huegemea kwenye kuulizana maswali), mwandishi anajenga hoja kwamba binadamu wote sio sawa. Ukiangalia utabaini kwamba binadamu hutofautiana katika mambo mengi tu – vipaji vyao, akili zao, hulka yao, maumbile yao, jinsia zao, rangi zao, imani zao, vipato vyao, vyeo vyao, makabila yao n.k. Pamoja na watu wote kutokuwa sawa, Mwalimu anaendelea, “bado kuna ‘minong’ono’ tuisikiayo moyoni kwamba watu wote ni sawa, na katika hadithi ya Binadamu kuna nyakati ambapo minong’ono hiyo imekuwa kelele iliyonyamazisha kila kitu.” Mwalimu anaendelea kunukuu mapambano ya, kwa mfano, Wamarekani kupingana na utawala wa Uingereza katika karne ya kumi na nane, Wafaransa kuupindua mfumo wa kifalme, Warusi kufanya mapinduzi dhidi ya dola ya kifalme, na kadhalika. Mwalimu ananukuu sehemu ya Tangazo maarufu la Uhuru wa Marekani isemayo:

> Twaamini Kanuni hizi kuwa ni dhahiri: kwamba watu wote wameumbwa sawa, na kwamba wamepewa na Muumba wao haki Fulani ambazo hawawezi kunyang’anywa, na kwamba baadhi ya haki hizi ni Uhai, Uhuru na Kutafuta Furaha.

Pamoja na kuandika hivyo, Mwalimu anadiriki kusema kwamba haamini kwamba mwandishi wa maneno haya, Bwana Thomas

Jefferson, aliamini, “na wala sikubali kwamba akina Yankee wanataka tuamini, kwamba kila M-yankee ni sawa na Jefferson katika madaha, ufasaha na akili, na kila askari wao ni sawa na George Washington katika ushujaa, uaminifu na huruma.” Na vilevile Wafaransa waliopiga kelele za “Uhuru! Usawa! Udugu!” hawakuamini wala hawakutaka kutuaminisha kwamba kila “Mfaransa ni sawa na Robespierre katika majivuno, akili na kupendwa … ”

Mwalimu anajumuisha hoja yake kwa kusema kwa msisitizo, “La, si dhahiri kwamba watu wote ni sawa.” Na anaongeza kwamba ili yale maneno yaliyomo kwenye Tangazo la Uhuru wa Wamarekani yawe sahihi zaidi ingefaa yaandikwe hivi:

> Twaamini Kanuni hizi kuwa ni dhahiri: kwamba ingawa watu wote si sawa wamepewa na Muumba wao haki Fulani ambazo hawawezi kunyang’anywa, na kwamba baadhi ya haki hizi ni Uhai, Uhuru na Kutafuta Furaha.

Hoja hizi zinamshawishi Mwalimu kuuliza, kama ni dhahiri kwamba binadamu wote sio sawa, nini ni chanzo cha “minongo’no” kwamba binadamu wote ni sawa. Katika sehemu ya pili ya makala yake, Mwalimu anatoa hoja za kichambuzi na kuainisha chanzo na msingi wa dhana ya “binadamu wote ni sawa”. Mwalimu anahitimisha kwa kusema kwamba, “Binadamu wote ni sawa katika ubinadamu wao.”

> Juma na Mwajuma hawahitilafiani katika ubinadamu wao. Katika mambo mengine yote Juma na Mwajuma si sawa, lakini katika ubinadamu wao hawahitilafiani hata chembe. Wewe huwezi, mimi siwezi, mtu mwingine ye yote hawezi, na wala Mwinyezi Mungu hawezi kumfanya Juma awe binadamu zaidi kuliko

> Mwajuma au kumfanya Mwajuma awe binadamu zaidi kuliko Juma. Mwinyezi Mungu aweza kufanya jambo ambalo wewe na mimi na wenzetu wengine hatuwezi kufanya – anaweza kumuumbua Juma na anaweza kumfanya Mwajuma awe kiumbe mwingine bora au hafifu zaidi kuliko binadamu, lakini hawezi kumfanya Juma au Mwajuma awe binadamu bora au hafifu zaidi kuliko binadamu wengine: hawezi kuongeza wala kupunguza ubinadamu wao.

Kwa kweli hitimisho hili la Mwalimu lina nguvu za kihoja na kimantiki na haliwezi kupingika kirahisi. Binadamu wote ni sawa katika ubinadamu wao, au kwa maneno mengine, katika *utu* wao. Na ubinadamu wa binadamu ni kitu pekee kinachomlinganisha binadamu mmoja na mwingine.

Inaelekea, sambamba na makala haya, au baada ya kuyakamilisha, Mwalimu alitunga shairi lenye kichwa cha habari 'Usawa wa Biandamu". Shairi hili vilevile limegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ikidhihirisha binadamu kutokuwa sawa, na sehemu ya pili ikibainisha kiini cha usawa wa binadamu. Anafungua sehemu ya kwanza kwa ubeti huu:

Wasema watu ni sawa, nambie usawa wao,
Kina hohehahe hawa, ambao hawana chao,
Na watu wenye vipawa, wenye vyeo wenye vyao,
Nambie usawa wao, watu mbalimlali hawa.

Katika sehemu ya pili, ndio anatoa beti zenye utamu wa hoja na uusanii. Ninashindwa kujizuia kunukuu beti hizi nne:

Watu ni sawa nasema, zingatia neno "watu",
Siwapimi kwa vilema, ambavyo ni udhia tu,
Siwafanidi kwa wema, ambao ni tabia tu,
Lakini watu ni watu, mawalii na wagema.

Niseme maji ni maji, pengine utaelewa,
Ya kunywa ya mfereji, na yanayoogelewa,
Ya umande na theluji, ya mvua, mito, maziwa,
Asili yake ni hewa, hayapitani umaji.

Yatie chumvi ya mvua, hayaachi kuwa maji,
Safi ukiyachafua, utakera tu wanywaji,
Yapashe moto, kwa jua, hayaongezi umaji,
Maji yoyote ni maji, maji nusu wayajua?

Binadamu kadhalika, wote kabisa ni sawa,
Si kwa nywele au rika, au wema na utawa,
Au huyu kusifika, Yule kudharaulika,
Ni wanAdamu na Hawa, asili ya kuumbika.

***

Kwa ufafanuzi huu wa dhana ya usawa wa binadamu, kwa maana ya ubinadamu au utu, ninadiriki kutoa hoja kwamba dhana ya Mwalimu ya usawa ni tofauti na dhana ya usawa katika mtazamo wa kibwanyenye. Usawa wa kibwanyenye hujikita kwenye dhana ya usawa wa kila mtu mbele ya sheria; Usawa mbele ya sheria kwa maana kwamba kila mtu ana haki sawa, yaani haki kwa maana ya *rights* au *equal rights*. Ingawa usawa wa Mwalimu pia una dhana ya haki ndani yake, neno 'haki' katika dhana ya Mwalimu ni kwa maana ya *justice* na sio *rights* tu. Ukiikubali dhana ya usawa wa binadamu kwa msingi wa ubinadamu wake, huwezi ukambagua binadamu yeyote katika kumtendea haki, yaani *justice*. Ukifanya hivyo utakuwa umeudhalilisha utu wake kwa sababu kutomtendea haki ni kinyume cha usawa wa binadamu. Kwa mantiki hiyo, unaweza ukawa sawa mbele ya sheria lakini huna haki sawa kutokana na kutokuwa sawa kijamii. Katika mfumo wa kibepari kila mtu ana haki sawa mbele ya sheria bila kujali hali yake halisi. Ukiwa tajiri au maskini wewe ni sawa mbele ya sheria lakini kila mmoja wetu anajua kwamba mwisho wa siku anayepata haki ni mtu mwenye uwezo. Kwa hivyo, usawa wa kibwanyenye unaweza

ukaendana na kutokuwapo usawa katika jamii na hali halisi, na ndivyo ilivyo katika mfumo wa kibepari. Lakini usawa katika dhana ya Mwalimu hauwezi kuhitilafiana kwa namna hii kwa sababu itakuwa kinyume na kiini cha usawa ambacho ni ubinadamu.

Hoja kama hizi ndizo zilizomsukuma Mwalimu kuupinga mfumo wa ubaguzi, ukoloni na hatimaye ubepari. Itikadi yake ya kijamaa ilijengwa kwa msingi wa usawa wa binadamu, yaani ubinAdamu wake na sio vinginevyo.

Mwalimu aliwahi kusema kwamba wajamaa wote duniani, hata wakitofautiana katika itikadi zao na mitazamo yao, bado hawawezi kutofautiana katika imani yao kuwa binadamu wote ni sawa. Yaani, huwezi kuwa mjamaa bila kuwa na imani hii. Hii ni sahihi kabisa. Lakini kinyume chake, sio wote wenye imani ya usawa wa binadamu ni wajamaa. Ubwanyenye unaweza kuwa na imani ya usawa, lakini ni usawa wa mfumo wa haki mbele ya sheria. Usawa wa kijamaa hujikita kwenye mfumo wa haki ya kijamii.

Tofauti ya msingi kati ya wajamaa ni kuhusu jinsi ya kujenga mfumo wenye haki ya kijamii. Mtazamo wa Ujamaa wa Kimarx husisitiza kwamba, mosi, ili kujenga mfumo mbadala hakuna budi kubomoa mfumo wa kibepari na, pili, huwezi kubomoa mfumo wa kibepari na kujenga mfumo wa kijamaa bila mapambano ya kitabaka. Wajamaa wengine huamini kwamba mfumo wa kijamaa unaweza kujengwa bila mapambano ya kitabaka kwa kuchukua tu hatua mbalimbali za kisheria. Mijadala kati ya mitazamo hii miwili miongoni mwa wajamaa ni sehemu ya historia ya Binadamu ya kutafuta usawa na uhuru wa binadamu.

Ujamaa wa Kimarx unajikita kwenye misingi mikuu mitatu, Moja, ni kwamba gurudumu la maendeleo ya historia ni mapambano ya kitabaka. Pili, kwamba katika jamii ya kibepari kuna matabaka mawili ya msingi: tabaka la wamiliki wa nyenzo za uzalishaji ambalo

hutumia nyenzo hizo kuwafanyisha kazi tabaka la wasio na nyenzo na kwa hivyo kuchuma faida ambayo hutokana na jasho la wafanyishwa kazi. Kwa maneno mepesi, tunaweza kuainisha matabaka haya mawili kama tabaka la wavujajasho na tabaka la wavunajasho.

Tatu ni kwamba ujamaa utajengwa na tabaka la wavujajasho kwa sababu maslahi na matamanio yao ni kujikumboa kutokana na unyonyaji. Na ukombozi huu wa kijamii hauwezi kupatikana bila mapambano dhidi ya tabaka tawala la kiuchumi ambalo hujilinda kupitia dola yao yenye kuhodhi vyombo vya mabavu – polisi, jeshi, magereza n.k. Kwa ufupi basi, Wanamarx hujikita kwenye kuleta mapinduzi kwa maana ya mabadiliko ya kimsingi katika mfumo wenyewe wa uzalishaji.

Kwa upande mwingine, mrengo wa ujamaa wa kiliberali au wa kidemokrasi hujikita kwenye kuleta mabadiliko katika mfumo uliopo kwa kutumia njia mbalimbali za mageuzi (sio mapinduzi), kwa mfano, sheria, elimu, n.k. Wao huamini kwamba unaweza kuwabadilisha wanyonyaji kwa kuwahubiria uzuri wa ujamaa kwa upande mmoja, na kuwadhibiti kupitia sheria, kwa upande mwingine.

Tofauti kubwa kati yao ni uelewa wao wa chombo-dola. Wanamarx husimamia kwenye hoja kwamba dola ni chombo cha mabwanyenye katika mfumo wa kibepari. Wajamaa wa kidemokrasi huamini kwamba chombo-dola ni chombo kisichoegemea au kufungana na tabaka lolote na kinaweza kutumika kuleta mabadiliko. Mwalimu alikuwa muumini wa mtazamo huo wa ujamaa wa kidemokrasi na alijaribu kwa dhati na nia nzuri kutumia chombo-dola kuleta na kujenga ujamaa.

Lakini kama alivyopenda kunukuu yeye mwenyewe: “Hata njia ya kwenda jahannamu imetandikwa na nia njema.” Nia njema bila

mapambano ya binadamu haziwezi kuleta mabadiliko makubwa na yenye manufaa kwa binadamu wote.

*Nitafarijika mno ikiwa nitaruhusiwa kubadilisha masomo yangu kutoka shahada ya sayansi na kwenda shahada ya sanaa. ….. Ninahisi, tena kwa dhati kabisa, kuwa ntakapomaliza masomo yangu, nitakuwa na mchango mkubwa zaidi kwa nchi yangu ikiwa nitasomea shahada ya sanaa na siyo ya sayansi. Jambo moja nina hakika nalo – nalo ni kuwa nina uwezo mkubwa zaidi wa kusoma shahada ya sanaa kuliko ya sayansi. Mwalimu wangu mmoja ambaye amenifahamu kwa miaka mingi, nikiwa mwanafunzi na baadae nikiwa mwalimu, alivosikia kuwa nakuja huku kusoma sayansi, alisema "Lo! hiyo ni kama kufinyanga kinyago kwa kutumia kalamu!" Nina hakika hakumaanisha kuwa mimi ni mpumbavu, lakini ananifahamu, na anajua anachokisema.*

- Mwalimu Nyerere Aprili 1949

(akimwandikia Mkurugenzi wa Elimu ya Makoloni, London)

# Mwalimu: Mwanazuoni Mkanushi

***Saida Yahya-Othman***
*Profesa Mshiriki Mstaafu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*
*saida.yahyaothman@gmail.com*

Mwandishi mmoja alimtumia Mwalimu kitabu chake mwaka 1981, akimuomba maoni, kwa vile aliamini kuwa Mwalimu alikuwa ni "mwanazuoni mahiri". Mwalimu alimjibu, "Mie si mwanazuoni yakhe". (Mengi yanayowasilishwa hapa kama nukuu hayakusemwa hivyo neno kwa neno, lakini maana ilikuwa hiyo, na nimejaribu kuwasilisha kama nukuu ili kuchangamsha makala). Unyenyekevu huu wa Mwalimu tumezoea kuusikia; ni taswira inayotawala. Na ni sahihi kabisa - tumesikia mara lukuki kuwa Mwalimu alikuwa mtu wa watu - akiweza kuongea na watu wa kawaida wa aina zote. Rafiki yake mkubwa, kwa mujibu wa wengi, alikuwa Mzee Dossa Azizi, ambae hakuwa na elimu kubwa wala utaalamu wa hali ya juu. Mwalimu alikataa tena na tena juhudi zote, na wakati mwengine hila, za kumvika kofia ya utukufu au kumtwaza umaarufu. Wakitaka kuzipa barabara jina lake, aliwaambia, "Hapana, hapana", ingawa walishindwa kuheshimu matakwa yake baada ya kifo chake. Walipotaka kujenga barabara ya lami kwenda Butiama, Mwalimu alishangaa: "Kwa nini, kwani wananchi wengine hawahitaji barabara za lami?" Na la waandishi kutumia jina lake kwenye vitabu ndo alikuwa analikwepa zaidi. Mshairi mmoja alimpelekea Mwalimu utenzi aloupa jina la *Nyerere na Uhuru wa Tanganyika*. Mwalimu alifurahia sana ule utenzi, lakini Jina Lake? "Hapana bwana! Uhuru wa Tanganyika inatosha. Hiyo Nyerere ya nini tena?" Pia Judith Listowel alipotaka kitabu chake *The Making of Tanganyika* kiwe na sehemu ya maisha ya Nyerere, Mwalimu aliudhika sana. "Sitaki sitaki kabisa. Andika historia ya nchi, mie nilikuwa mmoja tu wa wahusika, kwa nini unipe sehemu maalum?" Akadiriki hata kumshtumu Listowel kupenyeza "kwa mlango wa nyuma" sehemu za maisha yake yeye Mwalimu, akimaanisha

makubaliano yao ya awali yalikuwa tofauti. Katika mwaka wa mwisho wa maisha yake, wakati Jeshi na Serikali walipokuwa wanamkabidhi nyumba yake mpya na kubwa pale Butiama, Mwalimu alisema: “He! Jumba kubwa namna hii la nini? Kwani mie tembo?” Na alipokuja kuwa Rais, miaka ile ya mwanzo, alipoona zile mbwembwe na ving’ora na misafara ilokuwa ikipamba safari zake nje ya Ikulu, na kuwapa adha wananchi kwa kusimamishwa kwa muda mrefu huku msafara wake ukipita, aliandika barua kwa wizara na ofisi za chama zote, akilalamika:

> Ofisi ya Rais, kwenye jamhuri hii au yo yote ile, inabeba majukumu na madaraka ya Mkuu wa Nchi. Haitakiwi, na haipaswi, kumgeuza mshika ofisi hiyo kuwa chanzo cha usumbufu mkubwa kuliko wote katika mji mkuu wake.

Kwenye unyenyekevu huo taswira ni bapa, haibadiliki sana. Lakini kwenye usomi, uanazuoni, hali ilikuwa tofauti. Kwa upande mmoja, unyenyekevu na huko uliendelea. Siyo tu alisisitiza kuwa yeye si mwanazuoni, lakini mara nyingi akipenda kusema, wakati wa kutoa hotuba zake, “Mie sifahamu sana masuala haya, nafahamu kidogo tu”, na baada ya hapo kuendelea kuchambua kwa undani masuala hayo, na kudhihirisha uelewa wa kina kabisa. Na wanafunzi wazamili walivyomuandikia kumkosoa katika tafsiri yake ya Julius Caesar, Mwalimu alifuata ushauri wao, na katika toleo la pili akatoa shukrani zake kwenye dibaji.

Shaaban Robert na Mwalimu walikuwa marafiki, na ingawa Robert alikuwa mshairi bingwa kupita wote Tanzania, alikuwa mara nyingi anamtumia Mwalimu mashairi yake ayatolee maoni. Wakati Mwalimu akifanya ziara zake za harakati za kupigania uhuru katika miaka ya ’50, alikuwa akitafuta muda wa kupitia mashairi ya Robert na kumtumia maoni yake.

Naam, Mwalimu alikuwa mnyenyekevu juu ya uanazuoni wake, ambao, kwa hisia zake, hata hakuwa nao. Lakini matendo yake na maisha yake yote alikuwa anaupalilia na kuujenga uanazuoni, hadi watu wengine, hususan wanazuoni, kumuona ni mmoja wao kinda kindaki, na kumuweka katika kundi la wanafalsafa, wachambuzi na watafakari wa kiwango cha juu sana. Na ndio uhalisia wa uanazuoni. Uanazuoni hauji isipokuwa kwa kazi kubwa, na unapokuja, hauwezi kuganda; lazima uendelezwe kwa njia hai katika jamii. Mwalimu aliukuza uanazuoni wake kwa njia tatu.

Mosi, alisoma, na kusoma. Mwalimu hakupenda vitabu, alikuwa na *mahaba* na vitabu. Akivisoma, na kuvichambua, na kuvirarua. Msaidizi wake Mama Joan Wicken alikuwa na kazi kubwa ya kutafuta na kuagiza, mara nyengine hata kuomba, vitabu kwa marafiki na waandishi. Bajeti ya Ikulu ilikuwa finyu, na hasa fedha za kigeni, kwa hivyo Mwalimu hakuwa na uhuru mkubwa wa kununua kila kitabu alichokitaka. Bahati nzuri, wale waliomuona Mwalimu kuwa mwanazuoni mwenzi wao, walikuwa wanammiminia vitabu kama zawadi. Nae hakuwaangusha. Aliwashukuru, na kuahidi kuvisoma, au kuwambia kuwa ameshasoma na kutoa maoni yake. Alikuwa anakwepa kutoa mawazo juu ya miswada, sababu yake ikiwa, kwa vile yeye hakuchangia kwenye matayarisho ya miswada hiyo, alikuwa hana haki ya kuitolea maoni. Yumkin akihofia waandishi hao kutumia jina lake kuhalalisha maoni yao, au kuyapa umaarufu maandishi yao. Mara moja moja alivunja mwiko huu. Kijana wa Kitanzania alipompelekea utenzi kwa maoni yake, Mwalimu alimuandikia kumwambia utenzi wake mzuri sana na unastahili kuchapishwa, na yeye angeweza hata kusaidia katika jitihada hiyo. Lakini kitabu kikishachapishwa alikuwa hasiti kutoa maoni yake. Wakati mmoja Mwalimu alikuwa anatembelewa na mwanahabari wa Kijapani ambae alikuwa balozi wa heshima wa UNICEF, lakini pia aliwahi kuandika kitabu juu ya maisha yake wakati akisoma shule ya msingi Japani. Mama Wicken alipomjulisha Mwalimu kuwa huyo mama

anakuja kumtembelea, Mwalimu alisema “Ala, kumbe! Ndo nimo nasoma kitabu chake. Bahati kubwa hii, ntapata kuzungumza nae juu ya kitabu, ambacho nimekipenda sana.”

Wakati mwengine, Trevor Huddleston, ambaye alikuwa askofu wa Masasi kwa miaka minane kuanzia 1960, alipokuja kwenye sherehe za miaka 10 ya uhuru, alimletea Mwalimu kitabu kama zawadi. Huo ulikuwa wakati wa shughuli nyingi mno, Mwalimu akiwa kwenye hekaheka za kukutana na wageni na kuhudhuria sherehe mbalimbali. Lakini wiki mbili baadae, Huddleston alivyokwenda kumuaga Mwalimu, alishangaa sana pale Mwalimu alivyomwambia, “Rafiki yangu, kile kitabu nimeshakimaliza na nimekifurahia sana. Laiti tungekuwa na muda wa kuongea kidogo!” Lakini katika vitabu vyote Mwalimu alivyokuwa akisoma, vitabu vya riwaya vilikuwa havimkongi moyo. Akivisoma kwa nadra sana.

Pili, Mwalimu aliandika. Kinyume na viongozi wengine ambao walipokelewa kama wanafalsafa, kama vile Leopold Senghor wa Senegal, au Kwame Nkrumah wa Ghana, Mwalimu hakuwahi kuandika kitabu kimoja, ambacho pekee kiliweka wazi falsafa yake ya kisiasa na kijamii. Badala yake aliandika hotuba nyingi sana, na makala mafupi kama vile sehemu ya Kujitegemea katika *Azimio la Arusha*, na katika miaka ya karibu zaidi, kitabu kilokuja kuwa janga kwa baadhi ya wagombea uchaguzi mwaka 1995 - *Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania*. Kwa hivyo falsafa yake ya ujamaa imetoholewa kutoka maandishi yake haya, na amekuwa akiikuza na kuiendeleza kila miaka ilivyopita. Hotuba zake nyingi zimechapishwa kwenye vitabu vyake vya *Uhuru*, lakini nyingi nyengine alizitoa bila ya kuziandika, ukiondoa mistari miwili mitatu aliokuwa anaandika kwenye kijikaratasi.

Mwalimu alikuwa mhutubu na msemaji wa shani, hadi mwanahabari mmoja maarufu, Robin White, akasema kuwa ana “ulimi wa fedha”. Akiweza kuwavuta wasikilizaji wake wakacheka

nae, wakashangaa nae au wakalia nae. La kushangaza ni kuwa kumbe aliingiwa na hofu kubwa kabla ya kutoa hotuba, hasa za kimataifa. Alikuwa hawezi kula kabla ya hotuba, na tumbo likimtetemeka. Kweli muonekano wa juu unaficha mengi- nani angewaza, ingekuwa mwenyewe hakutamka, kuwa Mwalimu alikuwa na "hofu ya jukwaa"! Na hotuba zake hakuziandika bila ya kufanya utafiti wa kina juu ya mada husika. Ingawa walishirikiana kwa karibu sana na Mama Wicken katika kuandika, Mwalimu alitoa mawazo ya msingi, na baada ya Mama Wicken kuandika rasimu, Mwalimu akiipitia na kujadili na Mama Wicken kwa undani. Mara nyingi alikuwa anakataa mialiko ya kutoa hotuba, na pia mialiko ya muda mfupi, kwa sababu ingemnyima muda wa kutosha wa kutayarisha hotuba murua. Hii haina maana kuwa alikuwa hayuko tayari kuongea, hapana. Kuongea tu hakukuwa na tatizo. Wakati mmoja alialikwa Chuo Kikuu cha Namibia. Akawambia: "Kama mnataka nije kutoa hotuba sitaweza. La mnataka nije tuongee, mniulize masuali, na kadhalika, hapo sawa." Alipofika, aliongea kwa saa moja na nusu, na wasikilizaji wake walimshangilia sana. Aliongea, hakuhutubia.

Katika kuonyesha mapenzi yake (au mahaba mengine?) kwa lugha ya Kiswahili, na kubainisha uwezo wa Kiswahili kubeba dhana nzito za kisanii na kibunifu, Mwalimu alitafsiri vitabu vya Shakespeare *Julius Caesar* na *Merchant of Venice*, na kile cha Plato cha *Republic*. Alivipa majina ya *Juliasi Kaizari, Mabepari wa Venisi* na *Jamhuri*. Kazi zake za tafsiri zilianza tangu wakati wa kupigania Uhuru; kila akipata wasaa kidogo akitafsiri mistari miwili mitatu. Na kazi hii pia aliifanya kwa uadilifu mkubwa sana. Rasimu baada ya rasimu zikiandikwa na kuwekwa pembeni. Kazi ilikuwa ngumu zaidi kwa vile kazi za Shakespeare zilikuwa kwenye mfumo wa kishairi. Katika kutayarisha toleo la pili la *Juliasi Kaizari,* Mwalimu aliingiza masahihisho mengi ambayo aliyapata kwa wasomaji wake.

Tatu sasa, katika ukuaji wa uanazuoni wa Mwalimu - alidadisi na kuchambua kwa undani yale aliyokuwa akisoma na kuyaona. Na hapa ndipo unyenyekevu ulipoteleza kidogo. Mwalimu alikuwa hawezi kuwavumilia wapumbavu. Tusi lake kubwa ni kumwita mtu "mpumbavu", na ndio maana mara nyingi akitofautisha baina ya wajinga na wapumbavu. Wakoloni Waingereza, na baadae wanazuoni na masahibu wake wengine, walikiri kuwa Mwalimu alikuwa na kiburi cha usomi, au cha kizuoni. Kwa mtu ambae alikana uanazuoni wake, Mwalimu hakusita kuutambua na kuutunisha umahiri wake wa fikra na uchambuzi. Akifurahia sana mijadala ya kizuoni. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilishuhudia midahalo na Mwalimu mara nyingi alipokuwa Mkuu wa Chuo. Miaka ya '50 na '60, alikuwa na tabia ya kukutana na wanazuoni na waandishi wa kimataifa pale Cosy Cafe iliyokuwa Mkwepu Street, na kujadili nao kwa saa nyingi. Kuna hadithi ya yeye na Henry Kissinger, alipotembelea Tanzania mwaka 1976, walipokuwa wanarushiana nukuu za Shakespeare na wanafalsafa wengine wa Kiyunani. Mmoja wao akianzisha nukuu, mwengine akiimaliza, nenda rudi, nenda rudi. Mwishowe Mwalimu alirusha nukuu ya mwandishi mmoja wa Kimarekani. Kissinger aliduwaa kwa sekunde, kisha alicheka sana, "Ala! Huyo ni mimi bwana!"

Lakini kiburi cha Mwalimu kilituna zaidi kwa wale aliowadhani ni makasuku - waigizaji wa fikra za wengine - waliojaribu kupandikiza fikra hizo, ikiwa kutoka Mashariki au Magharibi, bila ya kutafakari na kuzingatia muktadha wa Tanzania na Afrika. Kwa sababu ambazo zinahitaji uchunguzi zaidi, Mwalimu alitapakaza pilipili ya kiburi chake cha kizuoni hususan kwa WanaMarx. Kwa hao, ulimi wake wa fedha uligeuka na kuwa wa siki. Aliwashutumu kuwa wakikasuku tu maandishi ya Marx na kauli mbiu zake, bila ya kuelewa, na bila ya kuchambua uhusiano wa fikra zake na jamii ya Kitanzania na ngazi ya maendeleo iliyofikiwa. Wakiimba wimbo, aliwambia, na kucheza ngoma ambayo wao wenyewe hawakuifahamu. Na waliwasulubu wale ambao walikuwa na fikra

tofauti. Mijadala ilikuwa mikali baina yake na wanafunzi na walimu wa Chuo Kikuu miaka ya 60 na 70. Mwalimu akisema yeye akimsoma Marx, na mengi ya Marx aliyapokea, lakini “upumbavu” na ukasuku wa WanaMarx wa Tanzania hakuweza kuuvumilia. Kiburi cha kizuoni cha Mwalimu kiliwavunja moyo WanaMarx kwa wakati ule. Hawakuamini kuwa mwanazuoni mnyenyekevu kama Mwalimu angeweza kugeuka na kuwa fidhuli kwa wanazuoni wenzake kwa kiwango kile. Angekuwa Kwame Nkrumah yu hai, angewambia, “Ala! Hamkujua! Niulizeni mie!”

Hiyo mada ya wakati mwengine. Mwalimu, mwanazuoni mkanushi.

*Kaizari:* *Ningekuwa kama wewe, ninge'za kushawishika,*
*Ningeshawishi kwa sala, sala zingenishawishi:*
*Bali mimi ni imara kama nyota ya shemali,*
*Il'o na hali ya kweli, imara yenye kituo,*
*Wala haina kifani huko kote uwinguni.*
*Uwingu umepambika kwa nyota bila idadi,*
*Ambazo zote ni moto na zote hutoa nuru;*
*Bali kuna nyota moja miongoni mwazo zote*
*Ikaayo pale pale.*
*Na dunia kadhalika ina watu wengi sana,*
*Nao wote wana mwili, wana damu na akili:*
*Bali miongoni mwao namjua mmoja tu*
*Ambaye hakanushiki, hukamata pale pale,*
*Na wala hatikisiki: na mtu huyo ni mimi,*
*Nitaonyesha kidogo, angao kwa jambo hili –*
*Niliamuru imara kuhamishwa kwa Simberi*
*Na bado niko imara abakie huko huko*

\- Mwalimu Nyerere 1963

(Juliasi Kaizari, tafsiri ya William Shakespeare, Julius Caesar)

# Mwalimu Mshairi

***M. M. Mulokozi***
*Profesa Mstaafu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili,*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*
*mugyam@gmail.com*

Tangu kale, ushairi wa Kiswahili ulioandikwa na ule ulionenwa kwa mdomo (simulizi), ulifungamana na maisha ya jamii katika hali zake zote – kitamaduni, kisiasa, kijeshi, kiuchumi, kielimu, n.k. Kwa lugha ya sasa, tungesema ushairi ulikuwa ndio “jukwaa la siasa” au “mtandao wa kijamii” ambamo watu wa aina zote na mitazamo anuwai waliwasiliana, kujadiliana, kuelimishana kuonyana, kukosoana na hata kupambana kwa kutumia kalamu na sauti zao. Muhimu zaidi, kwa madhumuni yetu ya sasa, ushairi wa Kiswahili (na hata wa makabila yetu yote) ulifungamana na harakati za siasa.

Washairi wengi wa kale wanaokumbukwa na kuheshimiwa sana walikuwa ni wanasiasa wapiganaji pia. Mifano ni Fumo Liyongo (karne ya 13), Zahidi Mngumi (mtawala wa Lamu, karne ya 18), Muyaka wa Muhaji (mtetezi wa Mombasa dhidi ya utawala wa Oman, kama 1776-1840), na Hemedi Abdallah (mpiganaji katika vita vya Abushiri dhidi ya Wadachi – 1888-89).

Mwalimu Julius K. Nyerere hakuibuka tu na kuwa mshairi na mpenzi wa lugha ya Kiswahili, bali aliibukia ndani ya jadi hiyo ndefu ya uanazuoni wa kimapambano wa Waswahili.

Akiwa mwanafunzi Makerere, Nyerere alishiriki katika mashindano ya uandishi wa insha na kutunukiwa tuzo ya uandishi bora kwa insha yake iliyohusu uhuru wa wanawake mwaka 1942. Miaka ya 1950, Nyerere alipoanza kufundisha katika shule ya sekondari ya Pugu, yumkini alifundisha pia somo la Kiswahili, maana tunajua kuwa alishiriki katika kuandaa mitaala na kuandika vitabu vya

kufundishia Kiswahili kwa kuombwa na serikali ya wakoloni. Haya yanaelezwa kwenye kitabu cha marehemu Erasto Mang'enya *Discipline and Tears.* Mang'enya alifuatana na Nyerere kwenda Iringa kwenye warsha ya kuandaa vitabu hivyo.

Wakati wa kuanzisha chama cha TANU mwaka 1954, miongoni mwa washirika na marafiki wakuu wa Nyerere walikuwa ni washairi. Baadhi yao ni Kaluta Amri Abedi (huyu walifahamiana tangu walipokuwa wakisoma wote Tabora), Saadani Abdu Kandoro, Mwalimu Mwalimu Kihere (mjomba wake Shaaban Robert), Khamisi Amani Khamisi (Nyamaume), Akilimali Snow-White, Mzee Waziri Kijana na Salehe Kibwana, bila kusahau washairi wanawake kama Mariamu Khamisi na Mwazamu Yange. Mwalimu alifahamiana pia na Shaaban Robert na Mathias Mnyampala, ambao hawakuweza kushiriki waziwazi katika siasa kwa kuwa walikuwa watumishi wa serikali. Kutokana na uhusiano wake wa karibu na wazee wa Dar es Salaam, na hasa washairi, mwalimu alijifunza Kiswahili kizuri na utunzi wa mashairi. Na alijiunga na kuwa mlezi wa chama cha washairi cha UKUTA kilipoanzishwa mwishoni mwa miaka ya 1950.

Mwalimu Nyerere alitambua mapema uwezo wa lugha ya Kiswahili wa kuunganisha Umma wa Watanganyika (na wa-Afrika Mashariki), na nguvu ya fasihi (pamoja na ushairi) katika kuhamasisha na kuelimisha Umma. Alianza kutunga mashairi miaka ya 1950. Kwa maelezo yake mwenyewe, alijifunza Kiswahili na utunzi wa mashairi kutoka kwa mabingwa, wakiongozwa na Amri Abedi. Katika "Utangulizi" wa *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Washairi* cha Mathias Mnyampala 1965, Nyerere anawataja karibu washairi wote aliovutiwa na mashairi yao, na ambao wamechapishwa katika mkusanyo huo.

Uhuru ulipokaribia Nyerere aliungana na washairi wenzake kutunga mashairi ya kuukaribisha Uhuru huku akidokeza kuhusu

jamii mpya huru na isiyo na ubaguzi ambayo ingejengwa baada ya kujitawala. Shairi lake la "Kunakucha Kulichele, na Kulala Kukomele" linaakisi jambo hili; tunapolisoma tunapata hisia za mapambazuko ya enzi mpya!

Mwaka 1962 Nyerere alitunga shairi la kumlilia Shaaban Robert, ambaye alifariki tarehe 20/6/1962. Kipindi hicho ndipo alipofasiri kwa Kiswahili tamthilia ya William Shakespeare ya *Juliasi Kaizari (Julius Caesar*). Kadhalika alitunga mashairi kadha yaliyofafanua sera na mtazamo wake kuhusu masuala ya uhuru, umoja, usawa na ujenzi wa nchi. Baadhi ya mashairi hayo yalichapishwa katika magazeti na mikusanyo ya mashairi, mathalan *Mashairi ya Saadani* (S.A. Kandoro), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Washairi* (Mathias Mnyampala), na *Mwongozo wa TANU* (chama cha TANU). Baada ya Tanganyika kutangazwa kuwa Jamhuri, mwaka 1962 Nyerere alilihutubia Bunge la kwanza kwa lugha ya Kiswahili, na kwa njia hiyo akawa amekitangaza Kiswahili kuwa Lugha ya Taifa na Lugha Rasmi ya serikali yake. Baada ya Azimio la Arusha, Nyerere alifasiri tamthilia nyingine ya Shakespeare iitwayo *Merchant of Venice* na kuiita *Mabepari wa Venisi* – jina ambalo liliakisi itikadi ya Ujamaa aliyokuwa akiiamini.

Azimio la Arusha lilitangazwa mwezi Februari mwaka 1967. Lengo lake lilikuwa ni kujenga nchi ya Ujamaa na Kujitegemea. Mwaka 1968, Nyerere aliwaalika washairi Ikulu na kuwaomba watumie ushairi wao kuhamasisha watu kujenga Ujamaa. Mwenyekiti wa Chama cha Washairi, Mathias Mnyampala, aliitikia wito huo mara moja kwa kuanzisha fani ya mashairi ya kisiasa aliyoiita *Ngonjera.* Washairi wengine walifuata kwa kutunga mashairi mengi kuhusu Azimio na Ujamaa, ambayo yalichapishwa katika magazeti na kuimbwa redioni. Baadhi yalihaririwa na kuchapishwa baadaye katika vitabu, kama vile cha Grant Kamenju na Farouk Topan cha 1971, *Mashairi ya Azimio la Arusha*, na cha A. Abdalla cha 1977, *Mashairi ya Miaka 10 ya Azimio.*

Ni vigumu, na si sahihi, kutenganisha mashairi ya Nyerere haya na maandiko yake mengine, yale ya kisiasa (k.m. *Ujamaa* na *Azimio la Arusha)* na yale ya kifasihi (kwa mfano tafsiri za Shakespeare). Maandiko yake mengi yanaelekea kuwa na lengo lilelile la kufafanua maongozi ya kisiasa aliyokuwa akiyasimamia kwa lengo la kujenga Taifa jipya la wakulima na wafanyakazi lenye kuzingatia haki na usawa. Ndiyo maana katika shairi la "Chombo cha Taifa Letu" anasema:

Chombo cha Taifa letu,
Si sawa na vya wenzetu
Vyao vyataka Rubani
Aushike usukani
Awe na mabaharia
Wanaomsaidia….
Kila aliye chomboni (cha Taifa letu)
Baharia na Rubani,
Ni mvuta makasia,
Na mhimizaji pia:
Kwa shibe au kwa njaa,
Wanaishi kijamaa…

Si chombo cha wadoezi,
Wala si chombo cha wezi;
Si chombo chenye nafasi,
Kwa wagomvi na waasi,
Watu wazua fitina,
Au wadhabidhabina.

Hakina nafasi hata,
Kwa watu wenye matata;
Kila mtu baharia,
Avuta lake kasia,
Agombane baharini,
Lake atavuta nani?

Anachosema Nyerere hapa ni kwamba katika Taifa analotaka kulijenga watu wote watakuwa ni wafanyakazi, wazalishaji mali; hapatakuwa na wanyonyaji. Dhana hii inaunganika na ile ya "utawala wa haki" inayobebwa na tamthilia ya *Juliasi Kaizari* na "usawa" inayojadiliwa katika shairi la "Usawa wa Binadamu."

> Wasema watu ni sawa, nambie usawa wao,
> Kina hohehahe hawa, ambao hawana chao,
> Na watu wenye vipawa, wenye vyeo wenye vyao,
> Nambie usawa wao, watu mbalimbali hawa
>
> Mwone Mbilikimo huyu, na Mtusi wa Ruanda,
> Huyu kimo cha kibuyu, na kanzu yake ni gwanda,
> Yule ni kama mbuyu, pandikizi mtu panda,
> Kibuyu na kingaranda, ni kibuyu si mbuyu…
>
> Usawa wa binadamu, si usawa wa sarafu,
> (Hata sarafu fahamu, kuna safi, kuna chafu)
> Kina bibi, kina amu, sawa bila hitilafu,
> Usawao nakwarifu, ni wao u-bin-Adamu.

Kwa ufupi, tungo za Nyerere zinabeba falsafa yake ya haki, usawa na Ujamaa wenye utu bila mizozo ya kitabaka.

Tukitizama kwa ufupi sanaa ya Mwalimu Nyerere, kwa kawaida yeye alitumia lugha tamu na rahisi katika tungo zake. Alitaka tungo hizo zieleweke kwa mwananchi wa kawaida. Hili linadhihirika wazi katika mashairi yake.

Jambo jingine linalojidhihirisha ni ubunifu na upekee katika utungaji wake. Nyerere alifahamu kanuni za kijadi za utunzi wa mashairi, na amezizingatia katika baadhi ya tungo zake. Lakini vilevile alikuwa ni mbunifu asiyekubali kutawaliwa na kanuni. Alijaribu kuingiza ubunifu ndani ya maumbo ya jadi ya ushairi bila kuyabadilisha sana maumbo hayo. Katika tafsiri zake za

Shakespeare, aliingiza mtindo wa masivina *(blank verse)* ambao aliutumia Shakespeare, na ule wa *rhyming couplets* (tawili zenye vina) kama tunavyoona katika tungo za “Chombo cha Taifa Letu”, “Mebeberu Wathubutu” *(Mwongozo)* na *Tanzania! Tanzania!* Mfano:

*Tawili 1*

Si chombo cha wadoezi,
Wala si chombo cha wezi;

*Tawili 2*

Si chombo chenye nafasi,
Kwa wagomvi na waasi,

*Tawili 3*

Watu wazua fitina,
Au wadhabidhabina.

Utunzi wa aina hii haukuwa kawaida katika ushairi wa kijadi, na ulizua rabsha miongoni mwa wanazuoni ambayo hatimaye ilizimwa na Amri Abedi katika “Dibaji” aliyomwandikia Mathias Mnyampala kwenye Diwani yake ya *Waadhi wa Ushairi.*

Kuanzia mwaka 1973 uliibuka mgogoro wa utunzi wa mashairi kati ya matapo mawili: *wanajadi* au *wanamapokeo,* na *wanausasa* au *wanamapinduzi.* Wanausasa walitaka uhuru katika utungaji; kwamba maumbo mapya ya ushairi yasiyozingatia urari wa vina na mizani yaruhusiwe. Wanajadi walitaka maumbo ya ushairi yabakie kama yalivyopokewa kijadi. Mgogoro huo ulidumu kwa zaidi ya miaka kumi, na ulihusisha washairi wa aina zote: wananchi wa kawaida, wasomi na hata wanasiasa. Nyerere aliufuatilia kwa karibu mgogoro huo, ambao ulimhusisha pia mwandishi wa makala haya. Baadhi ya wanajadi wenye ushawishi wa kisiasa

walimwendea Nyerere na kumwomba auzime mgogoro huu kwa kutumia rungu la dola. Nyerere alikataa. Mwezi Machi mwaka 1990 kikundi cha watetezi wa lugha ya Kiswahili, akiwamo mwandishi wa makala haya, kilikwenda Msasani kuzungumza na Mwalimu Nyerere kuhusu maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Mwandishi wa makala haya alipotambulishwa kwake, Mwalimu alianza kujadiliana naye kuhusu suala la ushairi wa Kiswahili na mgogoro kati ya wanajadi na wanausasa, na akamalizia kwa kusema: "Ushairi wa Kiswahili unahitaji *perestroika*." [Wakati huo mageuzi katika Jamhuri ya Kisovieti (Urusi) yalikuwa yamepamba moto yakiongozwa na Rais Mikhail Gorbachev, ambaye alianzisha dhana ya *perestroika* – yaani mageuzi yaliyoambatana na ulegezaji wa mfumo wa kisiasa na kiuchumi].

Kauli hii ya Nyerere inabeba mtazamo wake kuhusu ushairi wa Kiswahili (na labda sanaa kwa jumla) – kwamba ni muhimu kuruhusu ubunifu uchanue kwa kutoa uhuru zaidi kwa washairi na wasanii. Na kwa hakika, mbali na kuwa na maudhui mapya kuhusu usawa na Ujamaa, tunaweza kusema kuwa kisanaa ushairi wa Nyerere unaakisi dhana hii ya *perestroika.*

*Hii ni rai yangu kwa kizazi kipya cha viongozi wa Afrika na Waafrika. Jengeni umoja wa Afrika mkiamini kwamba bila umoja, Afrika haitakuwa na mustakabali mwema…. Ninapinga utukuzwaji wa vinchi tulivyovirithi kutoka ukoloni na mataifa bandia tunayojaribu kuyajenga.*

*Sisi sote ni Waafrika tunaojitahidi kuwa Waghana au Watanzania. Inatia moyo kwamba hatujafanikiwa kutimiza utashi wetu. Huko Ughaibuni Ughana au Utanzania wetu hautambuliki. Kinachotambulika ni Uafrika wetu.*

Mwalimu Nyerere 1997
(akihutubia wakati wa maadhimisho ya miaka 40 ya uhuru wa Ghana)

# Julius Nyerere, Mmajumui wa Kiafrika

***Ng'wanza Kamata***
*Mhadhiri Mwandamizi*
*Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*
*ngkamata@hotmail.com*

Wakati fulani mnamo mwaka 1958 Julius Nyerere, wakati huo tayari akiwa ni kiongozi wa chama cha TANU, alikutana na Tom Mboya mjini Nairobi. Katika mazungumzo yao, anaandika Tom Mboya, wazo la kuunda Vuguvugu la Ukombozi wa Kimajumui wa Afrika kwa Nchi za Afrika Mashariki na Kati, yaani PAFMECA lilizaliwa. PAFMECA ikaasisiwa mwezi Septemba mwaka 1958 miezi michache kabla ya Mkutano wa Watu wote wa Afrika (All African Peoples' Congress) uliokuwa umeitishwa na Nkrumah, kiongozi wa Ghana. Lengo la PAFMECA lilikuwa kuvikutanisha vyama vyote vya ukombozi katika eneo la Afrika Mashraiki na Kati na kuratibu na kuimarisha nguvu katika mapambano yao. Mkutano uliozaa PAFMECA ulikuwa pia ni maandalizi ya wajumbe toka eneo husika la bara kwa ajili ya Mkutano wa Accra.

Mpaka wakati huo ambapo PAFMECA inaundwa huko Ghana, chini ya uongozi wa Nkrumah, ndio ilokuwa Mecca ya harakati za ukombozi wa bara la Afrika. Hii ikitokana na mtazamo wa kimajumui wa Kiafrika wa Nkrumah, ambae akiamini kwamba Uhuru wa Ghana ulikuwa ni hatua tu ya kufikia ukombozi wa bara zima la Afrika, na kwamba Ghana haiwezi kuwa huru kama sehemu nyingine Barani hazikuwa huru. Ni wazi kwamba katika kipindi hiki jina lililosikika na kuhusishwa sana na Umajumui wa Kiafrika ni la Kwame Nkrumah. Nyerere kama Mmajumui hakujulikana sana wakati huu. Kwa Nyerere, hata walipokuwa wanaunda PAFMECA msukumo ulikuwa namna ya kuunganisha na kuratibu mapambano

ya ukombozi na kusaidiana katika harakati hizo na sio ujenzi wa Afrika yenye serikali moja.

Nyerere alikuwa kiongozi wa Chama cha Ukombozi (TANU) ambacho katika kipindi kifupi toka kiasisiwe kilikuwa tayari kimejipatia umaarufu mkubwa. Asili ya TANU ilikuwa African Association, chama cha Waafrika kilichoasisiwa mwaka 1929, kilokuwa na mtazamo wa kuwafikiria Waafikra kama wamoja. African Association, kilikuwa na wanachama na matawi katika sehemu mbalimbali za koloni la Tanganyika na Zanzibar. Wenyewe katika African Association wakijitambulisha kama Waafrika weusi wasiojali asili, nchi, dini, wala kabila la mtu. Kuwa Mwafrika mweusi ilitosha.

Katika mfano mmoja wa mawasiliano baina ya T. Edward John Mwangosi [Honorary Secretary wa African Association Dodoma] na Katibu Mkuu wa African Association Dar es Salaam, anaandika hivi juu ya African Association:

> … nia yetu i pamoja na wale wote wanaopenda kutumia jina la "African Association". Chama hiki kina maana sana pana Africa kwa kuwa Wa-Africa wengi ni mataifa mbali-mbali – wa kenya, Uganda, Nyasaland, Belgium Congo na Tanganyika tena kati yao kila watu wanajaribu kuweka chama chao kwa taifa lao au kwa Dini yao bali African Association ni Chama cha Wa-Afrika wote wa pande zozote na wadini yeyote na kabila lolote na wasio dini wastaarabu na wasio wastaarabu mradi wakiwa weusi wa Africa.

Pamoja na kwamba African Association hakikuwa chama cha kupigania uhuru lakini kilikuwa na mtazamo mpana wa Uafrika. Na tayari katika mwaka 1946 kilikuwa kimeanzisha mawasiliano na

Shirikisho la Wamajumui wa Kiafrika (The Pan-African Federation) lililokuwa London, Uingereza, na mmoja wa viongozi wao akiwa George Padmore. Tofauti ya dhana ya Mwafrika ya African Association na ya Nyerere ni kuwa wakati kwa African Association Mwafrika ni mtu mweusi kwa Nyerere Mwafrika ni mtu yeyote aliyechagua kuishi na kupafanya Afrika nyumbani kwao. African Association ilijikita zaidi kwenye umoja wa watu weusi bila kujali dini, kabila na tofauti nyingine, lakini sio moja kwa moja kwenye umajumui. Hata hivyo, tokea mapema, Nyerere, akiwa bado mwanafunzi pale Makerere, alikuwa na mahusiano na mawasiliano na baadhi ya watu wa African Association. Na mmoja kati ya watu hao ni Mwangosi ambaye anamtaja kama mtu aliyemshauri aanzishe tawi la African Association pale Makerere badala ya kuanzisha chama kipya. Hapana shaka kuwa fikra za umajumui wa Kiafrika za Nyerere zilitokana pia na kusoma na kufuatilia kwake vuguvugu la umajumui wa Kiafrika kwa wakati huo.

Nyerere hakuhudhuria Mkutano wa *All African Peoples Conference* ulioandaliwa na Nkrumah. Hili ni suala linalohitaji uchunguzi zaidi, ingawa wakati mkutano huo ukiandaliwa Tanganyika ilikuwa ikijiandaa kwa uchaguzi wa kwanza ambao ungeipa Tanganyika Serikali ya Madaraka (Responsible Government). Hii ilifanya Nyerere, mpaka wakati huo, asijulikane sana katika nyanja za mijadala ya kimajumui wa Kiafrika. Lakini tokea mwaka 1961, mara tu baada ya Tanganyika kupata uhuru wake, Nyerere alianza kuchomoza kama kiongozi mmajumui wa Kiafrika na Tanganyika ikaanza kuipiku Ghana kama Mecca ya wapigania uhuru barani. Ni wakati huo ambapo Nyerere alianza kuzungumzia masuala yasiyoihusu nchi yake tu bali nchi nyengine za Kiafrika. Hii iliinua nafasi yake kama msemaji na mtetezi wa nchi za Kiafrika. Msimamo wake juu ya Tanganyika kuwa au kutokuwa mwanachama wa Jumuiya ya Madola kama Afrika Kusini, chini ya ubaguzi wa rangi, ingeruhusiwa kuwa mwananchama ulivutia hisia za wafuatiliaji wengi wa mambo barani.

Vuguvugu la ukombozi lilikuwa limepamba moto na mikutano na majadiliano ya kuunda umoja wa Afrika yalikuwa yameshika kasi. Makundi tofauti yenye kujumuisha nchi mbalimbali za Kiafrika yalizuka na yakachukua misimamo iliyokinzana juu ya aina ya umoja wa Kiafrika unaotakiwa na namna utakavyofikiwa. Nkrumah aliongoza kundi la nchi lililoamini kuwa wakati wa Afrika kuungana ulikuwa umefika huku kundi jingine, ambalo baadae Nyerere ndio aliibuka kama kinara wake katika kulielezea, likichagiza kuwa wakati ulikuwa bado na sharti waende pole pole. Ni katika mijadala juu ya vuguvugu hili ambapo fikra za Nyerere juu ya umajumui wa Kiafrika zilipoanza kuchomoza wazi wazi.

Mtazamo wa Nyerere juu ya umajumui wa Kiafrika umejikita kwenye maeneo makuu sita. Kwanza, kwamba umoja ndio njia pekee ya kuharakisha na kuleta uhuru wa nchi za Kiafrika; pili, kwamba umoja huo huo ndio njia pekee itakayoisaidia Afrika kujiletea maendeleo yake, na hivyo kupambana na maadui ambao akiwaongelea sana - ujinga, maradhi na umaskini; tatu, kwamba umoja ndio njia pekee itakayoihakikishia Afrika usalama na uhuru wake kamili; nne, wakati gani umoja wa Afrika uundwe, na kwa njia au namna gani umoja huo utafikiwa; tano, ni nani hasa ataongoza jitihada za kuihimiza na kuisukuma Afrika iungane; na sita, pindi Afrika itakapoungana umoja huo utachukua sura gani hasa. Katika azma hizi Nyerere hakutofautiana sana na wenzake; tofauti kubwa ilikuwa kwenye wapi pa kuanzia – kutoka umajumui kwenda utaifa, au kutoka utaifa kwenda umajumui.

Kuhusu umoja na suala la ukombozi Nyerere aliamini kuwa ili kuharakisha ukombozi wa Afrika umoja ulikuwa ni lazima. Kwake yeye umoja ulikuwa ni silaha muhimu dhidi ya ukoloni na ubeberu. Lilikuwa ni suala la kimantiki tu kutambua kuwa pale watu wanapogundua kuwa na tatizo linalowakabili kwa pamoja, punde hugundua kuwa suluhu yake itapatikana kwa wao kushirikiana. Chimbuko la mtazamo huu linatokana kwa kiasi kikubwa na uzoefu

wake wa kuendesha harakati za ukombozi katika Tanganyika, koloni ambalo chama kimoja tu kilichipuka na kupevuka huku kikiungwa mkono na sehemu kubwa ya umma wa Watanganyika. Nyerere alitaka kuuelekeza uzoefu huu katika ngazi ya bara na kwenye mradi wa kuunda umoja wa Afrika bila mafanikio makubwa. Kwa upande mmoja alichukulia mambo kwa wepesi bila kuzibaini tofauti za kijamii na kisiasa katika kila nchi, na kwa upande mwingine, hakuzibaini nguvu za ubeberu na jitihada zake za kukwamisha ajenda yoyote yenye lengo la kuleta ukombozi wa kweli kwa Waafrika.

Wakati nchi za Afrika zilipokuwa zikipata uhuru dunia ilikuwa kwenye vita baridi, na wakoloni wakiandaa watawala ndani ya Afrika watakaowaendesha nyuma ya pazia kwa mtindo wa ukoloni mamboleo. Kwa hivyo kulikuwa na hali ya kutiliana mashaka ya nani ni nani na yuko upande gani katika siasa hizi za dunia. Mathalani pale Tanzania ilipochaguliwa na kuafiki kuwa mwenyeji wa Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika, Nkrumah alipinga kwa sababu akimtilia mashaka Nyerere kuwa ni kibaraka wa nchi za kibeberu. Hoja ya Nkrumah ilichochewa na kuitwa kwa majeshi ya Uingereza nchini Tanganyika kuja kusaidia kuzima maasi ya wanajeshi mwaka 1964.

Nyerere aliamini kwamba mapambano dhidi ya ukoloni yalikuwa ni kwa ajili ya kuwawezesha Waafrika kujiamulia mambo yao wenyewe na kwa hivyo kujiletea maendeleo yao wenyewe. Uhuru ulitakiwa kuwasaidia Waafrika kupambana na wale maadui wakuu wa maendeleo. Lakini alibaini kuwa hakuna nchi ya Kiafrika peke yake ambayo ingeweza kufanikiwa katika vita hii bila kushirikiana na nchi zingine za Kiafrika. Kwenye barua aliyomwandikia Mzee Kenyatta, Rais wa Kenya, mwaka 1963, Nyerere anabainisha kwamba Tanganyika ilitaka Shirikisho la Afrika Mashariki baada ya kugundua kuwa dola ya Tanganyika ilikuwa dhaifu mno kama nyenzo ya kukamilisha mapinduzi yaliyoanzishwa na mapambano

ya uhuru. Na kwa maoni yake ukweli huu ulikuwa ni dhahiri kwa nchi zote barani Afrika. Hii ilitokana na ukweli kwamba hata baada ya nchi za Afrika kupata uhuru rasilimali zake nyingi ziliendelea kushikiliwa na kuthibitiwa na nchi za kibeberu na makampuni yao.

Nyerere pia alibaini kuwa hali ya udunishwaji wa maendeleo ya nchi za Afrika (underdevelopment) ilidhoofisha jitihada zozote za nchi za Kiafrika za kujiletea maendeleo yao wenyewe. Na hii ilikuwa hivyo kwa sababu ya mfumo wa biashara ya kimataifa kutokuwa sawa na hivyo kuinyonya tu Afrika. Kutokana na uduni wa maendeleo yake, nchi nyingi za Afrika ni tegemezi na hushindana katika kutafuta misaada na upendeleo toka nchi tajiri na zenye nguvu. Njia pekee ya kupambana na hali hii, Nyerere alipendekeza, ni umoja ambao utaiwezesha Afrika kuzitumia rasilimali zake kwa manufaa yake. Katika fikra hizi Nyerere hakutofautiana sana na Nkrumah japo Nkrumah alilitazama suala hili kwa upana na kina na katika muktadha wa siasa-uchumi wa kibeberu.

Uduni wa maendeleo ya nchi za Kiafrika na utegemezi wao kwa nchi za kibeberu unazipunguzia, kama sio kuziondolea kabisa, uhuru (sovereignty) nchi za Kiafrika. Mbali ya hoja ya kiuchumi, Nyerere anakwenda mbali zaidi na kuangalia uwezo mdogo wa nchi moja moja ya Kiafrika katika kupambana na hila za mataifa makubwa za kuzigawa na kuzigombanisha kwa maslahi ya ubeberu. Na kwa sababu hiyo aliona umoja wa nchi za Kiafrika kama ndio njia pekee ya kuimarisha uhuru na usalama wao. Katika maisha yake yote, aliamini kuwa ‘vinchi’ vidogo vidogo vya Afrika visingekuwa huru bila kuunganisha nguvu zao kwa kuunda Serikali moja ya Afrika.

Baada ya kudurusu fikra na mtazamo wa Nyerere kuhusu umajumui wa Kiafrika, jambo moja linajitokeza - nalo ni kwamba fikra zake zinatokana na utambuzi na hisia za utaifa ndani ya mipaka ya ukoloni. Hisia hizi zinaweza kuwa na sura mbili. Moja ni

ile ya kutambua kwamba Waafrika wa Tanganyika walikuwa wananyonywa, kudhalilishwa, na kupuuzwa ndani ya ukoloni; lakini hali hiyo hiyo iliwakabili Waafrika katika makoloni mengine pia, na hivyo ili kuondosha upuuzwaji na udhalilishwaji wa Mwafrika wa Tanganyika sharti kukomesha udhalilishaji wa Waafrika katika bara lote. Kwa hivyo umoja ulikuwa ni njia muhimu sana katika kuharakisha uhuru wa kila nchi na kukomesha madhila haya. Na sura ya pili ni utambuzi kuwa 'vinchi' vidogo vidogo vya Afrika na dola zake havikuwa kitu chochote mbele ya mataifa tajiri na ya kibeberu. Na hivyo njia pekee ya kukabiliana na hali hiyo ilikuwa ni umoja. Hii ni tofauti na Nkrumah ambaye toka awali aliitazama Afrika kama ilitarajiwa kupambana na kupata uhuru ikiwa kama moja. Ndio maana hata pale Ghana ilipopata uhuru wake mwaka 1957 Nkrumah alisema uhuru wa Ghana haukuwa na maana yoyote kama Afrika yote haikuwa huru. Ni tofauti pia na chimbuko la umajumui wa Kiafrika, ambalo lilikuwa na itikadi ya umajumui wa watu, siyo madola. Dhana ya awali ya umajumui wa Kiafrika ilikuwa mshikamano zaidi kuliko umoja – mshikamano katika kuongoza madai ya watu weusi ya utu, usawa na kutokubaguliwa.

Aidha Nyerere alionesha hofu yake kuhusu mipaka iliyoachwa na wakoloni kuwa itakuwa chanzo cha migogoro baina ya nchi za Kiafrika na kuzidhoofisha zaidi. Ili kuepuka hilo aliona umoja kama njia pekee itakayosaidia kuepusha migogoro hiyo kwa sababu hakutakuwa tena na mipaka baina ya nchi za Kiafrika.

Pamoja na imani yake kubwa katika umajumui wa Kiafrika Nyerere hakuamini kabisa kwamba umoja wa Afrika unaweza kutokea haraka na mara moja kama alivyoamini Nkrumah. Msimamo huu wa Nyerere ulianza kujidhihirisha zaidi mara baada matumaini ya kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki kupotea kabisa. Ukichunguza kwa makini hoja alizotumia Nyerere kushawishi viongozi wenzake katika Afrika Mashariki ili wakubali kuundwa kwa shirikisho, utabaini kuwa zinafanana sana na hoja za Nkrumah za

kudai na kuhimiza kuundwa kwa umoja wa Afrika kwa haraka na mara moja

Katika kuhimiza kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki pendekezo la Nyerere lilikuwa ni kwamba shirikisho liundwe kabla ya nchi za Afrika Mashariki hazijapata uhuru wake. Kwa mara ya kwanza wazo hili lilitolewa na Nyerere katika mkutano wa PAFMECA mwaka 1960. Wakati huo ni Tanganyika pekee ndio ambayo ilikuwa na serikali ya madaraka na ndiyo pekee iliyokuwa ikijua tarehe ya uhuru wake toka kwa Waingereza. Lakini, kama inavyojulikana na wengi, Nyerere alikuwa tayari kuahirisha tarehe ya uhuru wa Tanganyika ili kusubiri nchi zote za Afrika mashariki ziweze kupata uhuru wao kwa pamoja zikiwa tayari zimeungana.

Moja ya sababu za hoja yake ya kuundwa kwa shirikisho kabla ya uhuru ni kwamba hisia za umoja zilikuwa kubwa na dhahiri zaidi miongoni mwa wapigania uhuru wakati wa harakati za kupigania uhuru kuliko wakati mwingine wowote. Vyama na viongozi wengi waliounda na kuongoza vuguvugu la kupigania uhuru wa nchi zao walikuwa tayari wamejenga ushirikiano mkubwa baina yao. Kwa hivyo ilikuwa rahisi kutumia vuguvugu hilo kuyaunganisha makoloni yote ya Afrika Mashariki chini ya Mwingereza. Aidha Nyerere alihofia kwamba mara baada ya uhuru viongozi wangejishughulisha zaidi na matatizo ya serikali zao na hatimaye kusahau faida kubwa itokanayo na umoja wa Afrika (au shirikisho); na kuwepo kwa maafisa wengi wanaotumikia nchi zao na kufaidika na maslahi na marupurupu yanayoambatana na vyeo vyao kungejenga kada kubwa zaidi ya wapinzani wa wazo la kuunda Serikali moja ya shirikisho kwa sababu tu ya kulinda nafasi na maslahi yao. Na jambo jingine ambalo aliliona lingeweza kuwa kikwazo, ni ugumu wa nchi kusalimisha mamlaka yake kamili (sovereignty) mara tu baada ya kuyapata.

Katika kubadilika kwake kifikra, na hasa alipoanza kuzungumza habari ya kufikia umoja hatua kwa hatua, Nyerere alisahau mambo haya muhimu na akapingana na Nkrumah kwa misingi hii. Hata hivyo karibu na mwisho wa miaka ya 1990 Nyerere alirejea hoja hii na kukaribia kukiri kuwa Nkrumah alikuwa sahihi. Miaka ya 1960 Nkrumah alisisistiza kwamba Afrika sharti iungane wakati ule, au sivyo haitaungana asilani kwa sababu utashi wa umajumui ungehama kutoka kwa watu na kujikita kwenye dola na viongozi wake. Yaani medani ya mapambano ya kimajumui ingebadilika.

Nyerere aliwashambulia waliodai kuwa muda wa kuunda Shirikisho ulikuwa bado; hawa aliwaita kina "bado kidogo", ambao wakidai kuwa uundwaji wa shirikisho kabla ya uhuru ungechelewesha uhuru wa kila nchi. Alishangaa vipi hoja iliyotumiwa na mabeberu kupinga kupatikana kwa uhuru wa nchi za Kiafrika kwa madai kuwa zilikuwa "bado kidogo" kupata uhuru kwa sababu ya ukabila, udini, na ukanda itumiwe na Waafrika wenyewe. Ndani ya Afrika mashariki hoja ya bado kidogo ilitokea Uganda, hasa miongoni mwa Wabaganda ambao wakihofia kumezwa kwa hadhi yao maalumu ndani ya Uganda na jumuiya kubwa itakayojumuisha muungano wa nchi nyingi.

Tofauti na alivyotarajia Nyerere, upinzani dhidi ya shirikisho la Afrika mashariki ulizuka kutoka ndani ya Afrika mashariki na kutoka sehemu zingine za Bara la Afrika. Msukumo wa wazi dhidi ya shirikiso kutoka nje ya Afrika mashariki ulitoka Ghana. Mwanahistoria Basil Davidson, katika kitabu chake cha *Black Star: A View of The Life and Times of Kwame Nkrumah* anabainisha kuwa Nkrumah, sio tu hakukubaliana na uundwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki lakini pia alifanya jitihada za wazi wazi za kuingilia na kujaribu kuuzuia mchakato wa uanzishwaji wake, jambo lililomkera sana Nyerere. Hoja ya Nkrumah dhidi ya Shirikisho la Afrika Mashariki ni kwamba ushirikiano wa kikanda ilikuwa ni namna nyingine ya kuigawa Afrika vipande vipande na kuchelewesha

umoja kamili wa Afrika yote. Nkrumah pia alitilia mashaka chanzo cha msukumo wa Shirikisho, na akimshuku Nyerere kuwa alikuwa akitekeleza matakwa ya nchi za kibeberu. Aidha, kwa mujibu wa chapisho maarufu la Chama cha Nkrumah, *Spark*, Shirikisho la Afrika Mashariki lilionekana kwenda kinyume na Makubaliano ya Addis Ababa yaliyoanzisha OAU.

Kuingilia kwa Nkrumah katika mchakato wa uundwaji wa Shirikisho kulizua malumbano makali baina yake na Nyerere. Mwezi Juni 1963 Nyerere alikuwa amewaandikia marais mbalimbali wa Kiafrika kuwajulisha juu ya azimio la viongozi watatu wa Afrika mashariki la kuunda shirikisho. Mmoja wa watu aliowatumia barua hiyo ni Nkrumah. Majibu ya Nkrumah kwa Nyerere yalimkasirisha sana Nyerere na kumfanya amjibu kwa hisia kali na za bezo. Katika baadhi ya majibu ya madai ya Nkrumah Nyerere alimshangaa Nkrumah katika kuamini kwake kuwa eti nchi tulizorithi kutoka ukoloni ndio ziwe nguzo muhimu ya umoja wa Afrika na nchi zinazoundwa kwa kuunganisha nchi kadhaa za Kiafrika ziwe kikwazo cha uundwaji wa umoja wa Afrika. Katika kuendelea kuteteta uundwaji wa Shirikisho, Nyerere alidai kuwa Shirikisho au umoja na Serikali za kikanda zinapunguza idadi ya nchi zitakazokuwa zikikutana kwenye mikutano ya OAU na kujadili suala la umoja, akiamini kuwa ni rahisi kufikia makubaliano mkiwa wachache kuliko mkiwa wengi. Kisiasa hili halikuwa tokeo la lazima kwani kama tulivyokwisha dokeza, pamoja na harakati za Nkrumah kukwamisha Shirikisho, siasa za ndani ya Uganda ziliifanya Uganda ianze kuvuta miguu kuelekea Shirikisho hata baada ya Waziri wao Mkuu, Milton Obote, kuwa ameshiriki katika mkutano uliopitisha azimio la kuundwa shirikisho.

Shirikisho la Afrika Mashariki halikupatikana kama ilivyoazimiwa. Hii illimfanya Nyerere kuanza kutilia mashaka nia na azma ya viongozi wote wa Kiafrika ya kuunda umoja kamili wa nchi za Afrika. Fikra hizi za Nyerere zilitokana na mosi, kitendo cha Nkrumah

kuingilia mchakato wa kuunda shirikishso, na pili, Nkrumah kuendelea kumshambulia Nyerere na kumsema kuwa alikuwa kibaraka wa ubeberu. Malumbano ya Nyerere na Nkrumah, hasa kwa njia za barua, yaliyoanza tokea mwaka 1960, yalifikia upeo wa juu pale Nkrumah alipoishambulia Tanganyika na Kamati ya Ukombozi ya OAU. Nkrumah hakuwa amekubaliana, hata huko nyuma, na Tanganyika kupewa heshima ya kuwa makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi. Ni katika Mkutano wa OAU wa Cairo wa mwaka 1964, ambapo Nyerere aliachana na hotuba yake iliyoandikwa na kujibu mashambulizi ya Nkrumah. Katika mashambulizi yake, Nyerere alihoji kama kweli Nkrumah alikuwa na nia ya dhati ya kuona bara la Afrika likiungana. Nyerere alisema kwamba wakati fulani alikuwa akifikiri kuwa viongozi wote barani Afrika walikuwa wana nia ya dhati juu ya suala la umoja. Lakini hapo alitamka wazi hofu yake kuwa si viongozi wote walikuwa na imani na nia hiyo kwa dhati. Alibainisha makundi mawili ya viongozi, wale waliotaka umoja wa Afrika kwa dhati kwa upande mmoja, na wale waliokuwa wakitumia hoja ya umoja kama propaganda. Hapana shaka Nyerere alimweka Nkrumah katika hilo kundi la pili, kwa sababu katika hoja hiyo pia alirejea jitihada za baadhi ya nchi zilizofanya hila ili kuzuia kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mtazamo wa Nyerere juu ya aina na muundo wa serikali ya Umoja wa Afrika au ile ya Shirikisho la Afrika Mashariki ni Serikali ya Shirikisho yenye nguvu na mamlaka kamili na makubwa. Alizitarajia nchi zote zilizokuwa tayari kuwa sehemu ya umoja wa Afrika kusalimisha kwa hiyari mamlaka yao kamili (sovereignty) kwa Serikali ya Shirikisho. Serikali hii ndio ingekuwa mwakilishi na msemaji mkuu wa masuala yote yanayoihusu Afrika kimataifa. Na serikali hiyo ingewajibika kutekeleza na kusimamia mambo yafuatayo - Mambo ya nje, Ulinzi, Uraia, Sarafu, Ushuru wa forodha, Biashara ya nje na Madini. Orodha ingeweza kuongezeka lakini haingekuwa pungufu ya mambo haya. Aidha Nyerere

alibainisha masuala mengine ambayo yangekuwa chini ya usimamizi wa pamoja wa mamlaka ya serikali ya shirikisho la Afrika na za kila nchi (concurrent list). Hata hivyo pale ambapo mgogoro ungetokea serikali ya shirikisho ndio ingekuwa na mamlaka ya mwisho. Msimamo wake huu kwa kiasi kikubwa ulifanana na ule wa Nkrumah.

Kwa muda mrefu suala la umoja wa Afrika lilihusisha zaidi viongozi wa kisiasa na maafisa waandamizi wa Serikali. Suala moja ambalo Nyerere hakulizungumzia sana, japo linajitokeza kwenye baadhi ya hotuba na maandishi yake, ni la nani hasa atasukuma mbele jitihada za ujenzi wa umajumui wa Afrika. Fikra zinazochomoza katika maandishi hayo ni kuwa dola au serikali ndizo zenye jukumu la kuendeleza jitihada za kuunganisha bara la Afrika. Mfano, alipokuwa anapingana na hoja ya waliotaka nchi zote za Afrika Mashariki zipate kwanza uhuru wao ili baada ya hapo kila nchi itafute ridhaa ya watu wake juu ya namna ya kujiunga na Shirikisho, Nyerere hakuona haja ya kufanya hivyo. Yeye alidhani ikiwa nchi zote zingekuwa zimefikia hatua ya Serikali ya Madaraka na zinazo wawakilishi katika Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO) kama ilivyokuwa Tanganyika mwaka 1959, ingetosha kuwauliza wawakilishi hao na jibu lao lingetosha kuhalalisha kuundwa kwa shirikisho. Na ndivyo ilivyokuwa wakati Tanganyika na Zanzibar zilipoungana mwaka 1964. Hata hivyo tofauti iliyopo kati ya LEGCO na Bunge la Tanganyika ni kuwa wapiga kura wachache zaidi walishiriki kuwachagua wajumbe wa LEGCO. Na haki ya kupiga kura nyakati zile ilibagua kwa vigezo vya elimu na mapato. Hivyo Watanganyika wengi hawakushiriki uchaguzi wa 1959. Lakini suali muhimu la kujiuliza ni kuwa katika jambo kubwa na muhimu kama hili iweje watu wasiulizwe?

Mwaka 1966 Nyerere alihutubia mkusanyiko wa wafanyakazi, wanataaluma na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Zambia. Na jambo moja alilolieleza ni mtanzuko (dilemma) anaokutana nao kiongozi

wa Kiafrika aliyeko madarakani ambaye pia ni mkereketwa wa umajumui wa Kiafrika. Kiongozi wa namna hiyo anaweza akajikuta akivutwa na masuala na matatizo ya nchi yake na hivyo kusahau au kutokuwa na muda wa kufikiria masuala ya umoja wa Afrika. Nyerere alidhani kuwa katika hali kama hiyo wenye jukumu la kuwafanya viongozi wa Kiafrika waendelee kufikiri na kuendeleza jitihada za ujenzi wa umoja wa Kiafrika ni wanataaluma na wanafunzi wa vyuo vikuu vya Kiafrika. Kwa hivyo hata katika hotuba hiyo Nyerere alikuwa anasema kuwa jukumu la msingi la kuleta umoja ni la viongozi wa serikali. Na kazi ya wasomi ni kuwakumbusha wakati wote juu ya jukumu lao hilo. Mantiki ya mtazamo huu, hasa kwa wasomi, imo kwenye nafasi ya vyuo vikuu na wanavyuo kwa maana ya wanataaluma na wanafunzi.

Lakini katika Tanzania jambo moja hatuwezi kulibeza. Japo Nyerere akiuona umajumui wa Kiafrika kama mradi wa dola, dola ya wakati wake angalau ilijitahidi kuwafunda vijana wa Kitanzania tokea mashuleni wakue wakiwa na fikra na mitizamo ya umajumui wa Kiafrika. Na kwa sababu ulikuwa ni mradi wa dola pindi dola ilipoachana na mradi huo mitazamo ya umajumui wa Kiafrika imedhoofu sana katika nchi zetu. Watu wengi na vijana katika bara la Afrika wamejaa fikra za utaifa, na kadri siku ziendavyo fikra hizo zinazidi kuelemea kwenye ukabila na udini. Suala la kuendelea kujadili kwa kina ni hili: Nani na vipi atahuisha na kusukuma mbele mapambano ya kuiendeleza ajenda ya umajumui wa Kiafrika?

# Marejeo

Abdalla, A., 1977. *Mashairi ya Miaka 10 ya Azimio.* Dar es Salaam: UKUTA.

Davidson, Basil, 1973. *Black Star: A View of the Life and Times of Kwame Nkrumah.* Oxford: James Currey.

Legum, Colin, 1964. *Pan Africanism: A Short Political Guide.* London: Frederick A. Praeger.

Listowel, J., 1963. *The Making of Tanganyika.* London: Chatto & Windus.

Mang'enya, E. A. M., 1984. *Discipline and Tears: Reminiscences of an African Civil Servant in Colonial Tanganyika.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mboya, Tom, 1986. *Freedom and After.* London: Andre Deustsch Limited.

Mnyampala, M., 1965. *Waadhi wa Ushairi.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Mnyampala, M., 1965. *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Dares Salaam: Chama cha Washairi wa Kiswahili.

Molony, Thomas, 2014. *Nyerere: The Early Years*. London: James Currey.

Nye, Joseph S. Jr., 1966. *Pan-Africanism and East African Integration.* Cambridge: Harvard University Press.

Nyerere, J. K., n,d. *Usawa wa Binadamu.* A poem reprinted in Saida Yahya-Othman & Bashiru Ally (eds.) 2015, *Kunakucha*

*Kulichele, na Kulala Kukomele: Mashairi Teule ya Mwalimu Julius Nyerere,* Kavazi Occasional Papers, no. 1: 9-12. Dar es Salaam: Nyerere Resource Centre, Tanzania Commission for Science and Technology.

------- 1974. *Freedom and Unity.* Oxford: Oxford University Press.

------- 1974. *Ujamaa ni Imani: Moyo kabla ya Silaha.* Dar es Salaam: East African Publishing House.

------- 1976. Transcript of President's Question and Answer Session with the Dar es Salaam University Students, 14th February 1976. SHC/PF/23/A State House files held at Mwalimu Nyerere Foundation, Dar es Salaam.

------- 1995. *Our Leadership and the Destiny of Tanzania.* Harare: African Publishing Group.

------- 2013. *Women's Freedom: Women are Eagles not Chickens.* Kampala: Fountain Publishers.

------- n.d. Watu Wote ni Sawa? Typescript in Nyerere's Butiama Library.

Pratt, Cranford, 1979. Tanzania's Transition to Socialism: Reflections of a Democratic Socialist. In Bismarck U. Mwansasu and Cranford Pratt (eds.) *Towards Socialism in Tanzania.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Shakespeare, W., 1969. *Juliasi Kaizari.* (Mfasiri: J. K. Nyerere). Toleo la pili. Nairobi: Oxford University Press.

Shakespeare, W., 1969. *Mabepari wa Venisi.* (Mfasiri: J. K. Nyerere). Nairobi: Oxford University Press.

Shivji, Issa G., 2014. *Utu, Usawa, Uhuru*: Building Blocks of Nyerere's Political Philosophy. In Leonhard Praeg & Siphokazi Magdla (eds.) *Ubuntu: Curating the Archive.* Grahamstown: University of Kwa-Zulu Natal Press.

Topan, F. na G. Kamenju, 1971. *Mashairi ya Azimio la Arusha.* Dar es Salaam: Longman.

In the Third World there is less concern and understanding about the problem of Peace and Nuclear Disarmament than in the Developed World. Similarly the Developed World has less concern and understanding about the problem of Development and Justice. I hope that your endeavour will increase understanding about both problem of Peace and Development in both "North" and "South"

Julius K. Nyerere.

Mwalimu Nyerere akiwa anasaini kitabu cha wageni wakati wa Mkutano wa Wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola (Commonwealth)